

**HOTUBA YA MHE. MAMA SALMA KIKWETE AKIZINDUA MAJENGO
YA VYUMBA VITANO VYA MADARASA NA VYOO VIWILI, SHULE YA
MSINGI WAZO HILL WILAYA YA KINONDONI, MKOANI DAR ES**

SALAAM,

TAREHE 29 APRILI, 2010.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ndugu William Lukuvi

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Ndugu Jordan Rugimbana

Mhe. Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Ndugu John Guninita

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Dar es Salaam, Bibi Zarina Madabida

Mheshimiwa Mbunge Jimbo Kinondoni, Ndugu Idd Azan

Wabunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam, Bibi Janet

Masaburi na Bibi Janet Kahama

Waheshimiwa Madiwani

Viongozi wote wa Chama na Serikali,

Walimu na wanafunzi, Mabibi na Mabwana,

Habari za leo!

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha wote kujumuika kwa pamoja wakati huu hapa Shule ya Msingi Wazo Hill.

Ndugu Viongozi, wanafunzi, Mabibi na Mabwana

Leo hii ni siku ya pili ya ziara yangu ndani ya Mkoa wa Dar es salaam. Napenda kuwafahamisha kuwa nina furaha sana kupata fursa hii ya kuwatembelea wanajumuia wote – walimu, wanafunzi, wafanyakazi mkiwemo na majirani wa Shule ya Msingi Wazo Hill.

Ni fursa pekee sana ya kuweza kubadilishana mawazo na kupeana ushauri kwa ajili ya kuboresha aidha kiwango au mazingira ya kitaaluma hapa shuleni, Mkoa wa Dar es Salaam na nchi nzima kwa ujumla.

Ndugu Viongozi, wanafunzi, Mabibi na Mabwana

Ili tuweze kupiga hatua katika vita ya kupambana na adui ujinga, hatuna budi kuwa na silaha muhimu zinazohitajika. Na kwa vita hii, pamoja na mahitaji ya msingi ya walimu, zana za kujifunzia na kufundishia, tunahitaji pia kuwa na miundombinu bora ya kutolea elimu. Ninaposema miundombinu ninamaanisha uwepo wa majengo muhimu kama madarasa, madawati na vyoo ili shule iwe na mazingira rafiki na yenye kuhakikisha usalama wa kiafya wa wanajumuia wote wa ndani na wale wanaoizunguka.

Ndugu Viongozi, wanafunzi, Mabibi na Mabwana

Napenda niwapongeze mno kwa mawazo, jitihada na ushirikiano uliowezesha kujengwa kwa vyumba vitano vya madarasa na vyoo viwili. Naomba nichukue fursa hii kuwatambua na kuwapongeza kwa mchango wenu kwa jamii, uliosababisha kuleta mazingira rafiki ya kujifunza na kufundisha katika shule hii. Ni matumaini yangu kuwa mtaendelea na moyo huu na pia nawaomba wadau wengine waguswe na suala hili nyeti la elimu ili nao waweze kuiga hili mlilofanya nyie hapa Shule ya Msingi Wazo Hill.

Ndugu Viongozi, wanafunzi, Mabibi na Mabwana

**NAPENDA NITAMKE RASMI WAKATI HUU KUWA MAJENGO HAYA,
MADARASA 5 NA VYOO 2, YAMEZINDULIWA RASMI KWA MATUMIZI
YAKE.**

Naomba niwaage kwa kuwatakieni kila la heri katika shughuli zenu
za ujenzi wa taifa!

Ahsanteni kwa kunisikiliza!